# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1025

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-831-6

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA UALIMU KWA VITENDO
# STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI

**2023**

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN: 978-9987-09-831-6

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 168/ +255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2023). *Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kupiga chapa, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo


Orodha ya Majedwali ........ iv

Vifupisho ........ v

Shukurani ........ vi

1.0 Utangulizi ........ 1

2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ........ 1

3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........ 2

3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu ........ 2

3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu ........ 2

4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali ........ 3

5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3

6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali, na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4

6.1 Mkufunzi ........ 4

6.2 Mwalimu tarajali ........ 5

6.3 Mzazi/Mlezi ........ 5

7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6

8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6

9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ........ 7

10.0 Idadi ya Vipindi ........ 8

11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 8

Bibliografia ........ 18

## Orodha ya Majedwali


Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Mwaka wa Kwanza na wa Pili ........ 3

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu ........ 7

Jedwali Na.3: Maudhui ya Mwaka wa Kwanza ........ 9

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Mwaka wa Pili ........ 13

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

# Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Elimu ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Ualimu kwa Vitendo ni la lazima kwa mwalimu tarajali wa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali. Lengo la kufundisha somo hili ni kumwezesha mwalimu tarajali kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Kupitia somo hili mwalimu tarajali ataweza kuandaa na kufundisha somo kwa ufanisi, kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji, kuandaa na kutumia zana za kufundishia na kujifunzia, kumtathmini mwanafunzi na kushughulikia changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, mwalimu tarajali ataweza kuchopeka masuala mtambuka katika masomo bebezi na kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Muhtasari huu umeandaliwa ili kumuongoza mkufunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Ualimu kwa Vitendo, Tanzania Bara. Aidha, muhtasari unatoa maelekezo yatakayomwezesha mkufunzi kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji ili kumjengea mwalimu tarajali stadi za udadisi, ubunifu, mawasiliano, ushirikiano, fikra tunduizi na utatuzi wa changamoto. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali wa Mwaka 2023 ambao una lengo la kumwandaa mwalimu mwenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazomwezesha kujitegemea na kutumia vyema fursa zinazopatikana nchini ili kuweza kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yake ya kila siku.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

Lengo kuu la elimu ya ualimu ni kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, na anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu ni kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;

(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;

(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mtoto;

(e) Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali wa mtoto mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na

(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-action based research*).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali

Umahiri wa jumla wa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali unalenga kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;

(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mtoto;

(e) Kutumia, TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kumtambua mtoto mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;

(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (*instructional leadership*); na

(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, *classroom-action based research).*

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa na mwalimu tarajali umeoneshwa katika jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Mwaka wa Kwanza na wa Pili*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu ya Awali | 1.1 Kuchambua mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu ya Awali |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 2.0 Kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Awali | 2.1 Kuandaa mazingira katika ufundishaji na ujifunzaji<br>2.2 Kuandaa zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>2.3 Kuandaa darasa salama, changamshi na jumuishi |
| 3.0 Kuwezesha ujifunzaji katika darasa la awali kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | 3.1 Kusimamia darasa katika ufundishaji na ujifunzaji<br>3.2 Kutumia sanaa na michezo kama nyenzo za ufundishaji na ujifunzaji<br>3.3 Kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>3.4 Kuchopeka masuala mtambuka katika malezi, ufundishaji na ujifunzaji<br>3.5 Kuchopeka matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Awali<br>3.6 Kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa darasa kubwa katika mazingira jumuishi<br>3.7 Kupima, kutathmini na kutoa mrejesho wa maendeleo ya ukuaji na ujifunzaji wa mtoto kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>3.8 Kutoa ushauri na unasihi katika malezi, ufundishaji na ujifunzaji wa mtoto |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali, na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na Ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mkufunzi, mwalimu tarajali na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile

zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki.

## 6.2 Mwalimu tarajali

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ufundishaji na ujifunzaji, mbinu za kufundishia na kujifunzia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na changamoto za ujifunzaji ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia, kuandaa na kutumia zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kumtathmini mwanafunzi.

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

## 6.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi/ mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika ujifunzaji.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali unasisitiza matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi anapaswa kutumia mbinu shirikishi zitakazomwezesha mwalimu tarajali kujenga umahiri uliokusudiwa. Baadhi ya mbinu hizo ni nyimbo, hadithi, maigizo, michezo, oneshombinu, changanyakete, kisamafunzo, utafiti, kazimradi, matembezi ya garali, igizodhima, maswali na majibu, ziara ya mafunzo, bunguabongo na majadiliano katika vikundi. Mbinu hizi zitamwezesha mwalimu tarajali kuwa mbunifu, kufikiri kiyakinifu, kuwasiliana, kushirikiana, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali na kutatua changamoto mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji.

Mkufunzi anashauriwa kumwongoza mwalimu tarajali kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia mbinu shirikishi wakati wa mazoezi ya ufundishaji na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mazingira halisi na kuzingatia mahitaji ya mtoto.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji katika somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji ya ujifunzaji. Mkufunzi anapaswa kutumia zana zitakazomwezesha mwalimu tarajali kutumia mlango wa fahamu zaidi ya mmoja wakati wa ujifunzaji ili kumjengea tabia ya udadisi, ugunduzi na kukuza fikra tunduizi. Vilevile, mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka au kufaragua zana kwa kutumia makunzi/malighafi zinazopatikana katika mazingira yake. Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa ni pamoja na abakasi, dadu, sinia la namba, chati za namba na herufi, vibao fumbo, kadi za namba, herufi na picha, vihesabio, michoro ya picha mbalimbali, domino, ngoma, zeze, kayamba, kengele, filimbi, kinanda, zana mguso/mkwaruzo, kamusi ya lugha ya alama na alfabeti ya lugha ya alama. Aidha, mkufunzi anapaswa kuhakikisha kuwa mwalimu tarajali anapata nafasi ya kujifunza uandaaji na utumiaji wa zana mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji.

## 9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa somo la Ualimu kwa Vitendo utafanyika kwa kuzingatia vigezo vya upimaji wa maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujenzi wa umahiri. Mwalimu tarajali atapimwa kwa kufanya vitendo vya ufundishaji, ikiwamo kuandaa somo, kufaragua zana, kufanya mazoezi ya ufundishaji, kufanya upimaji endelevu na tamati na kutoa mrejesho.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Katika kuamua kiwango cha ufaulu wa mwalimu tarajali, upimaji wa mwisho (tamati) utachangia asilimia thelathini (30%) na upimaji endelevu utachangia asilimia sabini (70%). Kwa upande wa upimaji endelevu alama za mtihani wa muhula wa pili mwaka wa kwanza zitakuwa 10%, kazimradi ya ufaraguzi 15% na mafunzo kwa vitendo 45%. Aidha, alama za mafunzo kwa vitendo zitakazotokana na ufundishaji igizi zitakuwa 20% na ufundishaji katika shule za jirani 25%. Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia 50% na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafikisha 50%, mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama za upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2:** *Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| **Shughuli ya upimaji** | **Alama (%)** |
|---|---|
| Mtihani wa Muhula wa Pili Mwaka wa Kwanza | 10 |
| Kazimradi ya ufaraguzi | 15 |
| Ufundishaji igizi/kiduchu | 20 |
| Ufundishaji katika shule jirani | 25 |
| **Jumla** | **70** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika sitini (60). Idadi ya vipindi kwa somo hili ni kumi (10 ) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Somo la Ualimu kwa Vitendo Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika jedwali Na. 3 na 4.

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Awali | 1.1 Kuchambua mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu ya Awali | Kuaridhia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu ya Awali (*aina, umuhimu, matumizi na changamoto*) | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu ya Awali zimearidhiwa | Matini zinazohusu njia na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji na video zenye maudhui ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji | 10 |
| 2.0 Kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Awali | 2.1 Kuandaa na kutumia mazingira katika ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kuchambua dhana ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji | Dhana ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji imechambuliwa | Muhtasari wa somo, Vitabu vya kiada na ziada, mazingira halisi ya ujifunzaji, chati yenye kanuni za mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji na matini mbalimbali zenye maudhui ya somo husika | 68 |
| | | (b) Kubaini kanuni za kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji | Kanuni za kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji zimebainishwa | | |
| | | (c) Kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika miktadha mbalimbali | Mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yameandaliwa kwa kuzingatia miktadha mbalimbali | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kuandaa zana za ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia | Zana za kufundishia na kujifunzia zimetengenezwa | Makunzi yanayotumika kutengeneza zana husika mfano maboksi, vijiti, vipande vya mbao, gundi, rangi, kamba, misumari na udongo wa mfinyanzi<br>Picha na michoro ya zana husika<br>Boksi, kasha, sanduku, mifuko ya nailoni, turubai na kabati | 78 |
| | | (b) Kuhifadhi zana za ufundishaji na ujifunzaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zimehifadhiwa | | |
| | | (c) Kuandaa kivunge cha zana za ufundishaji na ujifunzaji | Kivunge cha zana za ufundishaji na ujifunzaji kimeandaliwa | | |
| | 2.3 Kuandaa darasa salama, changamshi na jumuishi | (a) Kupanga darasa kwa kuzingatia mazingira husika na mahitaji ya mtoto | Darasa limepangwa kwa kuzingatia mazingira husika na mahitaji ya mtoto | Picha ya mfano ya darasa lililopangwa kwa kuzingatia mazingira halisi na mahitaji ya mtoto<br>Zana za kufundishia na kujifunzia zilizofaraguliwa kwa | 64 |
| | | (b) Kupanga zana katika kona za ujifunzaji | Zana zimepangwa katika kona za ujifunzaji | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kuzingatia mazingira halisi na mahitaji ya mtoto mfano vitu halisi na mchoro/picha mguso<br><br>Picha ya mfano wa darasa lililopangwa zana katika kona za ujifunzaji | |
| 3.0 Kuwezesha ujifunzaji katika darasa la awali kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | 3.1 Kusimamia darasa katika ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kubaini mahitaji ya kila mtoto katika ufundishaji na ujifunzaji | Mahitaji ya kila mtoto katika ufundishaji na ujifunzaji yamebainishwa | Dodoso la ubainishaji wa mahitaji ya mtoto<br><br>Zana za ubainishaji wa mapema wa mahitaji ya mtoto<br><br>Video zenye maudhui ya kutumia kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji | 120 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuhamasisha ushiriki wa mtoto katika ujifunzaji | Ushiriki wa mtoto katika ujifunzaji umehamasishwa | Chati yenye kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji<br><br>Zana za ufundishaji na ujifunzaji mfano vitu halisi na picha/mchoro mguso | |
| | | (c) Kutumia kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji | Kanuni na taratibu za usimamizi wa darasa zimetumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji | | |
| | | (d) Kutumia mbinu na zana shirikishi, jumuishi na changamshi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji | Mbinu na zana shirikishi, jumuishi na changamshi zimetumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji | | |
| | 3.2 Kutumia sanaa na michezo kama nyenzo za ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kutumia sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji *(Ufundishaji igizi chuoni).* | Sanaa na michezo imetumika katika ufundishaji na ujifunzaji | Zana za michezo kulingana na mchezo husika mfano kamba, ngoma na filimbi | 60 |

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Mwaka wa Pili*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kuwezesha ujifunzaji katika darasa la awali kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | 3.2 Kutumia sanaa na michezo kama nyenzo za ufundishaji na ujifunzaji | (b) Kutumia sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji *(Ufundishaji wa darasa halisi na katika mazingira ya shule chini ya uangalizi wa mkufunzi/ mwalimu wa somo)* | Sanaa na michezo imetumika katika ufundishaji na ujifunzaji | Zana za michezo kulingana na mchezo husika mfano kamba, ngoma na filimbi | 46 |
| | 3.3 Kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | (a) Kufundisha kwa kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi | Mbinu, teknolojia na vifaa saidizi vimetumika katika ufundishaji | Zana na vifaa mbalimbali vya TEHAMA na teknolojia saidizi mfano tabuleti, kompyuta, runinga na projekta<br><br>Video zenye maudhui ya kutumia mbinu, teknolojia na<br><br>vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji | 36 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 3.4 Kuchopeka masuala mtambuka katika malezi, ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji | Masuala mtambuka yamechopekwa katika ufundishaji na ujifunzaji | Matini zinazohusu masuala mtambuka kama vile elimu jumuishi, maadili na ulinzi na usalama | 28 |
| | 3.5 Kuchopeka matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Awali | (a) Kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji | TEHAMA imetumika katika ufundishaji na ujifunzaji | Zana na vifaa mbalimbali vya TEHAMA na teknolojia saidizi mfano tabuleti, kompyuta, runinga na projekta<br><br>Video zenye maudhui ya matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji | 28 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 3.6 Kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa darasa kubwa katika mazingira jumuishi | (a) Kufundisha darasa kubwa na jumuishi kwa kutumia mbinu na zana shirikishi | Mbinu na zana shirikishi za kufundisha darasa kubwa na jumuishi zimetumika | Zana mbalimbali za kuona na kushika, vitu halisi na picha/ michoro mguso<br>Video zenye maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji wa darasa kubwa na jumuishi | 38 |
| | | (b) Kubuni shughuli zinazohusisha matumizi ya mlango wa fahamu zaidi ya mmoja | Shughuli zinazohusu matumizi ya mlango wa fahamu zaidi ya mmoja zimebuniwa | | |
| | 3.7 Kupima, kutathmini na kutoa mrejesho wa maendeleo ya ukuaji na ujifunzaji wa mtoto kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | (a) Kutumia mbinu na zana za upimaji, ikiwemo TEHAMA, katika kupima na kutathimini maendeleo ya ujifunzaji na ukuaji wa mtoto | Mbinu na zana za upimaji ikiwemo TEHAMA zimetumika katika kupima na kutathimini maendeleo ya ujifunzaji na ukuaji wa mtoto | Sampuli ya zana za upimaji na maendeleo ya ujifunzaji wa mtoto mfano hojaji, dodoso na mkoba wa kazi<br>Orodha hakiki ya kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji wa mtoto | 78 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji na ukuaji wa mtoto | Maendeleo ya ujifunzaji na ukuaji wa mtoto yamefuatiliwa | Daftari la kumbukumbu za maendeleo ya ujifunzaji na ukuaji wa mtoto<br>Mwongozo wa uchunguzi wa maendeleo ya ujifunzaji wa mtoto<br>Ripoti za maendeleo ya ujifunzaji wa mtoto | |
| | | (c) Kutoa mrejesho wa ujifunzaji wa mtoto | Mrejesho wa ujifunzaji wa mtoto umetolewa | | |
| | | (d) Kutumia taarifa za matokeo ya upimaji katika kuboresha utendaji, ufundishaji na ujifunzaji | Taarifa za matokeo ya upimaji katika kuboresha utendaji, ufundishaji na ujifunzaji zimetumika | | |
| | 3.8 Kutoa ushauri na unasihi katika malezi, ufundishaji na ujifunzaji wa mtoto | (a) Kubaini watoto wenye uhitaji wa ushauri na unasihi | Watoto wenye uhitaji wa ushauri na unasihi wamebainishwa | Mwongozo wa ushauri na unasihi<br>Ripoti za maendeleo ya ujifunzaji<br>Matini na video zenye maudhui ya kutoa ushauri na unasihi kwa mtoto kuhusu masuala yanayoathiri ujifunzaji | 46 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutoa ushauri na unasihi kwa mtoto | Ushauri na unasihi kwa mtoto umetolewa | | |

## Bibliografia


Brookhart, S. M. & McMillan, J. H. (Eds.) (2019). *Classroom assessment and educational measurement*. Routledge.

Brookhart, S.M. (2008). *How to give effective feedback to your students*. ASCD Publications.

Levin, J. & Nolan, J. F. (2000). *Principles of classroom management: A Professional decision-making model*. Allyn and Bacon.

Mohan, R. (2016). *Measurement, evaluation and assessment in education*. PHI Learning Pvt. Ltd.

Orlich, D. C., Harder, R. J., Callahan, R. C., Trevisan, M. S. & Brown, A. H. (2012). *Teaching strategies: A guide to effective instruction*. Cengage Learning.

Sood, N. (2016). *Guidance counselling education*. Vikas Publishing House Pvt. Ltd.

Souza B. (2021). *Teaching practice: A handbook for student teachers*. LAP Lambert Academic Publishing.

Sundaram, G. (2007). *Principles and practice of guidance and counselling*. Aavishkar Publisher Distributors.